OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA MASASI

SHULE YA SEKONDARI NDANDA

UKARABATI/UJENZI WA MIUNDO MBINU YA SHULE YA SEKONDARI YA NDANDA

Simu: 0737862646
Email:ndandasecondaryschool@gmail.com
Unapojibu tafadhali taja:

S. L. P. 10,
NDANDA.

Kumb: Na. NSS/B.7/2020/008

31/08/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA *'LOCAL FUNDIS'* UJENZI/UKARABATI

Kwa kusudi la kuimarisha ujuzi kwa vitendo kwa wanafunzi wa fani mbalimbali za ualimu kupitia vyuo vya ualimu nchini Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WyEST) kupitia mradi wa EP4R inatekeleza miradi ya kukarabati/kujenga miundombinu mbalimbali ya Shule Kongwe ya sekondari Ndanda.

Mradi huu unatekelezwa kwa mwongozo wa *'FORCE ACCOUNT'* wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia mtaalamu elekezi ambaye ni Chuo cha Ufundi Arusha *(Arusha Technical College-ATC)* na kamati za mradi *(Project Committees)*..

Hivyo Mwenyekiti wa kamati ya mradi wa Ujenzi wa shule ya sekondari Ndanda anawatangazia wananchi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi zilizoainishwa katika tangazo hili kuomba kazi katika fani zifuatzo:-

(I). FANI NA MASHARTI/SIFA MAHUSUSI ZA MAFUNDI ZINAZOHITAJIKA;

A. FUNDI UASHI, KUPAUA NA RANGI.

(1) Awe amewahi kufanya kazi inayofanana na kazi hii yenye thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua Tshs. 6,000,000.00 (Milioni sita) katika kipindi cha mwaka 2018 hadi mwaka 2020. Lazima aambatanishe nyaraka zifuatazo ili kuthibitisha kuwa ni kweli amewahi kufanya na kukamilisha mradi wenye thamani tajwa hapo juu:

(a) Mkataba wa kazi yenye thamani tajwa hapo juu

(b) Hati za malipo ya gharama za ufundi (payment certificate) katika kipindi cha mwaka 2018 hadi mwaka 2020.

(c) 'Bank Statement' ikionesha gharama za malipo ya ufundi aliyolipwa yenye thamani tajwa hapo juu katika kipindi tofauti tofauti kuanzia 2018 hadi mwaka 2020 kwa mkataba husika wa kazi hiyo.

(d) Barua pendekezwa (recommendation letter) kutoka kwa Mwenye mradi wa awali kwa kazi hiyo.

(2) Awe na mtaji wa kulipa mafundi bila kulipwa malipo ya awali (Advance Payment)

(3) Awe na uwezo wa kusoma michoro na kufanya makadirio ya mahitaji (materials).

(4) Awe na uwezo wa kujenga kwa tofali zote za block na za kuchoma.

(5) Awe na uwezo wa kupaua paa za aina mbalimbali katika majengo ya serikali.

(6) Awe na uwezo wa kupaua mabati ya aina zote na kufanya *'blandering & ceiling* ya aina ya *Alluminium false Suspended Ceiling'*

(7) Awe na uwezo wa kuweka sakafu za za aina mbalimbali (za kawaida,tiles,terrezo n.k).

(8) Awe na uwezo wa kutumia mitambo na vifaa mbalimbali vya ujenzi.

(9) Awe na timu ya kutosha ya mafundi wasaidizi na vibarua wenye weledi wa kazi.

(10) Fundi anaweza kuomba jengo zaidi ya moja kadri uwezo wake utakavyoruhusu.

(11) Fundi lazima awasilishe bahasha mbili tofauti ambazo ni bahasha ya nyaraka za maombi na bahasha ya bei na ataitwa katika usaili baada ya bahasha yake ya maombi kufunguliwa na kukidhi vigezo vya awali vya kiufundi vilivyowekwa katika Tangazo hili.

(12) Michoro na fomu za mchanganuo wa shughuli za ujenzi za mradi huu zinapatikana katika Ofisi ya Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi ya sekondari Ndanda.

(13) Fundi lazima aombe na kujaza kazi zote (Uashi, Kupaua na Rangi) kama ilivyooneshwa katika tangazo hili. Fundi ambaye ataacha kujaza kipengele kimojawapo miongoni mwa vipengele tajwa hapo juu (uashi,kupaua na rangi) maombi yake hayatafanyiwa kazi.

(14) Cheti cha ufundi ni sifa ya ziada kwa fundi husika.

B. FUNDI UMEME

(1) Awe amewahi kufanya kazi inayofanana na kazi hii yenye thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua **Tshs. 3,000,000.00 (Milioni tatu) katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2020 . Lazima aambatanishe nyaraka zifuatazo ili kuthibitisha kuwa ni kweli amewahi kufanya na kukamilisha mradi wenye thamani tajwa hapo juu.**

(a) Mkataba wa kazi wenye thamani tajwa hapo juu

(b) Hati za malipo ya gharama za ufundi (payment certificate) kwa kipindi cha mwaka 2018 hadi mwaka 2020 .

(c) 'Bank Statement' ikionesha gharama za malipo ya ufundi aliyolipwa yenye thamani tajwa hapo juu katika kipindi tofauti tofauti kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2020.

(d) Barua pendekezwa (recommendation letter) kutoka kwa Mwenye mradi wa awali.

(2) Awe na mtaji wa kulipa mafundi bila kulipwa malipo ya awali (Advance Payment)

(3) Awe na uwezo wa kusoma ramani/mchoro na kuitafsiri.

(4) Awe amesajiliwa na kupata Leseni kutoka Ewura

(5) Awe na uwezo wa kuweka mfumo wa kung' amua moto (fire detectors).

(6) Awe na uzoefu wa kufunga umeme katika majengo ya serikali na mitambo/mashine.

(7) Fundi anaweza kuomba jengo zaidi ya moja kadri uwezo wake utakavyoruhusu.

(8) Fundi lazima awasilishe bahasha mbili tofauti ambazo ni bahasha ya nyaraka za maombi na bahasha ya bei na ataitwa katika usaili baada ya bahasha yake ya maombi kufunguliwa na kukidhi vigezo vya awali vya kiufundi vilivyowekwa katika Tangazo hili.

(9) Michoro na fomu za mchanganuo wa shughuli za ujenzi za mradi huu zinapatikana katika Ofisi ya Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi ya shule ya sekondari Ndanda.

(10) Fundi lazima ajaze vipengele vyote vilivyoainishwa katika fomu ya mchanganuo wa gharama za ujenzi kwa majengo na miundombinu mbalimbali.

(11) Cheti cha ufundi ni sifa ya ziada kwa fundi husika

C. FUNDI BOMBA

(1) Awe amewahi kufanya kazi inayofanana na kazi hii yenye thamani ya jumla ya gharama za ufundi isiyopungua **Tshs. 3,000,000.00 (Milioni tatu) katika kipindi cha mwaka 2018 hadi mwaka 2020. Lazima aambatanishe nyaraka zifuatazo ili kuthibitisha kuwa ni kweli amewahi kufanya na kukamilisha mradi wenye thamani tajwa hapo juu:-**

(a) Mkataba wa kazi wenye thamani tajwa hapo juu

(b) Hati za malipo ya gharama za ufundi (payment certificate) katika kipindi cha mwaka 2018 hadi mwaka 2020.

(c) 'Bank Statement' ikionesha gharama za malipo ya ufundi aliyolipwa yenye thamani tajwa hapo juu katika kipindi tofauti tofauti kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2020.

(d) Barua pendekezwa (recommendation letter) kutoka kwa Mwenye mradi wa awali.

(2) Awe na uwezo wa kusoma michoro/ramani ya maji safi/taka na kuitafsiri

(3) Awe na uwezo wa kufanya makadirio ya mahitaji (materials) ya mfumo wa maji.

(4) Awe na uwezo wa kujenga/kutengeneza mfumo wa maji safi.

(5) Awe na uwezo wa kujenga/kutengeneza mfumo wa maji taka uliokamilika utakayojumuisha *'inspection chambers, sepetic & soak-way pits'*

(6) Fundi mmoja anaruhusiwa kuomba jengo zaidi ya moja.

(7) **Fundi lazima awasilishe bahasha mbili tofauti ambazo ni bahasha ya nyaraka za maombi na bahasha ya bei na ataitwa katika usaili baada ya bahasha yake ya maombi kufunguliwa na kukizdhi vigezo vya awali vya kiufundi vilivyowekwa katika Tangazo hili.**

(8) Michoro na fomu za mchanganuo wa shughuli za ujenzi za mradi huu zinapatikana katika Ofisi ya Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi ya shule ya sekondari Ndanda.

(9) Fundi lazima ajaze vipengele vyote vilivyoainishwa katika fomu ya mchanganuo wa gharama za ujenzi kwa majengo na miundombinu mbalimbali.

(10) Cheti cha ufundi ni sifa ya ziada kwa fundi husika

(II) MASHARTI YA UJUMLA KWA MWOMBAJI;

(1) Mwombaji **lazima** awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18.

(2) Mwombaji **lazima** aandike barua ya maombi kwa jina lake na siyo Kampuni au jina la biashara.

(3) Mwombaji **lazima** abainishe muda ambao atautumia kufanya kazi atakayoomba

(4) Mwombaji **lazima** aambatanishe barua ya mdhamini mwenye mali zisizohamishika na barua kutoka Ofisi ya Serikali ya Kijiji/mtaa.

(5) Mwombaji **lazima** awe na Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi(TIN number)/ Kitambulisho cha ujasiliamali.

(6) Mwombaji **lazima** awe na Akaunti ya benki **iliyo hai**.

(7) Kwa fundi ambaye anataka kuomba fani zaidi ya moja atalazimika kutuma barua mbili kwa kila maombi kwa fani hizo.

(8) Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya 'ki-eletroniki' na posta hayatapokelewa.

(9) **Cheti** ni sifa ya ziada kwa mwombaji.

(10) Mwombaji awe tayari kufanya kazi kwa awamu (shift) na siku za mwisho wa wiki (Jumamosi na Jumapili) itakapolazimika kufanya hivyo.

(11) Barua za maombi yote yawasilishwe kwa njia ya mkono Ofisi ya Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi ya shule ya sekondari Ndanda ambae ni mkuu wa shule yakiwa yameandikwa anuani ifuatayo:

Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi

Mradi wa Ujenzi/Ukarabati wa miundo mbinu ya shule sekondari Ndanda

S. L .P, 10

Ndanda.

(12) Mwisho wa kupokea Maombi ni tarehe **8/9/2020** saa **04:00** asubuhi ambapo boksi la wote walioomba litafunguliwa, tafadhali mnaombwa kuwepo wakati wa ufunguzi.

(13) Kila muombaji ahakikishe barua yake ya maombi ina namba yake ya simu inayopatikana muda wote

(14) Fundi atataarifiwa (kwa njia ya simu) siku ya tarehe ya usaili na Mwenyekiti wa mradi

(15) *Siku ya kutembelea na kuona eneo la ujenzi/ukarabati itakuwa ni Ijumaa ya tarehe 4/9/2020 na Jumamosi ya tarehe 5/9/2020 kuanzia saa 04:00 asubuhi mpaka saa 07:00 mchana. Tafadhali fika ofisi ya Mkuu wa shule ambae pia ni mwenyekiti wa kamati ya ujenzi.*

Tangazo hili limetolewa leo tarehe 31/08/2020 na

Morega S. Mongate

MWENYEKITI WA KAMATI YA UJENZI NA UKARABATI

SHULE YA SEKONDARI NDANDA

HEADMASTER
NDANDA HIGH SCH
P.O. BOX 10
NDANDA